TAREKHE YA WANAVYUONI WA ZANZIBAR

SAYYID AHMAD BIN HUSEIN AAL-SHEIKH ABU BAKAR BIN SALIM (1313-1385 AH)

SAYYID AHMAD BIN HUSEIN BIN AAL-SHEIKH

Jina lake

Sayyid Ahmad bin Husein bin Saleh bin Abubakar bin Ahmad bin Abubakar Ahmad bin Abubakar bin Abdallah bin Salim bin Abdallah bin Ali bin Sheikh Abubakar bin Salim Baalawy.

Kuzaliwa na kulelewa kwake

Sayyid Ahmad bin Husein amezaliwa Moroni (Ngazija) mwaka 1313 Hijria, alililewa huko kisha akasafiri kwenda Madagaska akiwa mdogo na baadae akafika Zanzibar akiwa na umri wa miaka 19.

Kusoma kwake

Alikuja Zanzibar kwa lengo la kusoma elimu za dini kwa Mashekhe wa zama hizo lakini baadae akaamua kufanya maskani yake hapo hadi kufariki kwake.

Amesoma kwa Mashekhe wengi lakini zaidi alichota elimu kwa Mabwana wafuatao:

1. Habib Ahmad bin Abubakar bin Sumeit.

2. Sheikh Abdallah bin Muhammad Bakathir.
3. Sheikh Said bin Dahman.

Na alimlazimu zaidi Sheikh Said bin Dahman hadi kufariki kwake.

Tariqa na Aqida yake

Alikuwa na Aqida ya Ahli Sunna Waljamaah akifuata Madhehebu ya Kishaafii na Tariqa ya Aal Baalawy. Na huu ndio mwenendo wa Wanavyuoni wengi wa Zanzibar tokea dahari na ndio hali za Mashekhe zake.

Hali zake za kila siku

Pamoja na kuwa alisoma kwa Mashekhe wakubwa na kufika daraja ya elimu kubwa kabisa lakini Sayyid Ahmad bin Husein hakuwa na darasa zilizokumbukwa na aliwaachia Mashekhe wenziwe waongoze Taaluma.

Sayyid Ahmad alipendelea zaidi njia ya UchaMungu kwa kuutumia muda wake mwingi kuleta dhikr, mazingira yake yalikuwa ni baina ya nyumbani kwake na Msikitini.

Kila siku alikuwa akiwepo Msikiti Jibril uliopo Mkunazini Zanzibar kuanzia adhuhuri kwa mchana kutwa akisali Sala zake hapo na kukaa Itikafu kwa kusoma nyiradi zake na visomo vyake. Baadae huwepo Msikiti wa Mwembetanga (jirani na nyumba yake) baina ya Magharibi na Isha na kuongoza nyiradi ikiwemo Ratibul Haddad.

Waislamu wa Zanzibar walimjuwa bwana huyu kwa UchaMungu wake hivyo wakimwelekea wapate dua zake kwa kila haja zao iwe sawa akiwa kwake nyumbani au Msikitini nae hakuwa akimrejesha mtu bila ya kumuombea dua.

Sayyid Ahmad pamoja na kuwepo kwake Msikitini muda mrefu lakini pia alikuwa ni mtu wa jamii akihudhuria shughuli zote zinazostahiki kuhudhuriwa mfano wa maziko, khitma, harusi, hawli na hadhara za nyiradi.

Sayyid Ahmad bin Husein alikuwa na Uradi maalumu akiufanya nyumbani kwake kila siku baada ya Sala ya Isha wakihudhuria watu makhsusi walio karibu nae na hugaiwa maji ya miwa kwa wanaohudhuria.

Miongoni mwa yaliyokuwa yakisomwa katika uradi wa Isha:

- يَا رَشِيْد Mara mia moja (100)
- يَا حَفِيْظ Mara mia moja (100)
- صَلَّى اللهُ عَلَى سَيِّدِنَا مُحَمَّد Mara mia moja (100)
- اَلفَاتِحَة - Kisha huombwa dua

Miongoni mwa waliokuwa wakihudhuria urahi huu:

1. Sayyid Omar bin Abdallah (Mwenyebaraka).
2. Sheikh Muhammad bin Salim Baabde.
3. Bwana Mfaume Seha.
4. Bwana Ahmed Himidi.

Imepokewa kutoka kwa waliomlazimu Sayyid Ahmad kuwa alipendelea sana anapoomba dua yoyote ile basi humalizia na dua maalum pia akiwahimiza watu waiombe na kuitolea Ijaza. Dua yenyewe ni:

- يَا أَوَّلَ الأَوَّلِيْنَ، وَيَا آخِرَ ٱلآخِرِيْنَ، وَيَا ذَا ٱلقُوَّةِ ٱلمَتِيْنَ، وَيَا رَاحِمَ ٱلمَسَاكِيْنَ.
- وَيَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِيْنَ (mara 3)
- وَيَا سَلاَم سَلِّمْنَا وَٱلمُسْلِمِيْنَ (mara 3)
- اَللَّهُمَّ أَحْيِنَا عَلَى ٱلإِسْلاَمِ وَالسُّنَّةِ، وَأَمِتْنَا عَلَى ٱلإِيْمَانِ وَالتَوْبَةِ، بِجَاهِ سَيِّدِ ٱلمُرْسَلِيْن.

Mambo mazuri aliyotuwachia

Sayyid Ahmad bin Husein pamoja na nyiradi nyengine alikuwa akijilazimu zaidi kuusoma Uradi wa "Ratibul-Attas" usiku na mchana na kila anapofikwa na haja.

Pia aliupangia uradi huu usomwe kila siku ya Alkhamis baada ya Sala ya Alaasiri katika Msikiti Jibril, walihudhuria waliokuwa wakimlazimu pamoja na watu wa kheri mbalimbali.

Msikiti Jibril ulikuwa ukinawiri kwa kujaa watu wa kila rika katika siku hii ya uradi wa "Ratibul-Attas" na ilikuwa ada kugaiwa sadaka kwa yeyote anayetaka kutabaruku kutoa sadaka.

Aliuongoza uradi huu wakati wa uhai wake wote kisha akapokewa na waliomfatia baada yake awamu kwa awamu hadi kufikia zama hizi pamoja na kuwa idadi ya wanaohudhuria ya sasa ni ndogo kulinganisha na ilivyokuwa katika zama zake.

Miongoni mwa waliompokea kuiongoza "Ratibul-Attas":

1. Sayyid Omar bin Abdalla Aal-Sheikh
2. Sayyid Ahmad bin Yasin.

3. Sayyid Ahmad bin Abbas Aal- Sheikh.
4. Sayyid Sheikh Al-Habshy.
5. Sayyid Muhammad bin Abbas Jamalul-Leyl.
6. Sayyid Abdurahman bin Sheikh Al-Habshy.

Nyiradi zinazosomwa Msikiti Jibril Laasiri kwa wiki:

1. Ratibul-Attas (kila siku ya Alkhamisi).
2. Hadhra ya Baa-Sawdaan (kila Jumanne).

1.Ratibul-Attas

Huu ni Uradi maalumu uliokusanywa na Mwanachuoni MchaMungu wa Hadhramout Habib Omar bin Abdurrahman bin Aqiil Al-Attas bin Salim bin Abdallah bin Abdurrahman bin Abdallah bin Sheikh Abdurrahman Saqqaf. Bwana huyu alifariki tarehe 23 Rabiul Aakhar 1072 Hijria na kuzikwa katika mji wa Hureydha (moja ya miji maarufu Hadhramout).

Uradi huu husomwa wakati wowote asubuhi na mchana na khasa panapotokezea shida, husoma kila mtu peke yake na pia husomwa kwa pamoja kama unavyosomwa Msikiti Jibril.

Baadhi ya faida za Uradi huu:

Uradi huu una Baraka na faida kubwa kwa mwenye kushikamana nao khasa asubuhi na jioni. Dhikri zilizomo ndani yake ni nzito na zenye kumkinga mtu na kila aina ya mabalaa.

Miongoni mwa faida zake:

1. Humkinga mtu na shari za aina zote zinazotoka kwa wanaadamu, majini, uchawi n.k na huenea kinga hiyo umbali wa nyumba 40 kutoka sehemu inaposomwa.
2. Huondoa khofu iyayotokana na jambo lolote baya.
3. Hukidhi haja.
4. Huondoa mikosi na mabalaa.
5. Husamehewa dhambi.
6. Hukunjua rizki, huondowa ukame na huondoa dhiki za maisha.
7. Hufanya takhfif ya maradhi.
8. Huifanya mali iwe salama (kutoibiwa au kuangamia).
9. Humzidishia mtu umri wake.
10. Humsababishia mtu kupata "Husnul-Khatima" n.k.

2. Hadhra ya Baa-Sawdaan.

Huu ni mkusanyiko wa nyiradi zilizokusanywa na Mwanachuoni Mchamungu aliyekuwa mji wa Do'an

Hadhramout Imam Abdallah bin Ahmad bin Abdallah bin Muhammad bin Abdurrahman Baa-Sawdaan Al-Kindy inarejea nasabu yake kwa Sahaba Al-Miqdad ibnil- Aswad Al-Kindy (R.A).

Alizaliwa mwaka 1178 Hijria na amefariki tarehe 7 Jamadil-Uula 1266.

Uradi huu pia husomwa kwa pamoja au mtu peke yake wakati wowote na kwa haja yoyote japokuwa umezoeleka kusomwa kwa pamoja kila siku ya Jumanne baada ya Sala ya Laasiri kama unavyosomwa Tareem (mji maarufu wa Hadhramout) na Msikiti Jibril kwa Unguja

Uradi huu ulikuwa ukisomwa Msikiti Helwa uliopo Kiponda kabla ya kuhamishiwa Msikiti Jibril. Katika Msikiti Helwa pia ukisomwa kila Jumanne Alaasiri na kuongozwa na Sayyid Aidarous bin Hassan Aal-Sheikh Abubakar katika miaka ya 50' mpaka 60' hadi ulipositishwa.

Kisha Sayyid Omar bin Abdallah (Mwenye Baraka) akauhuisha uradi huu na kuuhamishia Msikiti Jibril katika miaka ya 80' baada ya kukatishwa kusomwa kwa takriban ya miaka 20 na kurithiwa kuongozwa na watu wa kheri na kuhudhuriwa na watu wa rika mbalimbali.

Miongoni mwa walioongoza uradi huu wa Msikiti Jibril:

1. Sayyid Omar bin Abdallah (Mwenye Baraka)
2. Sayyid Sheikh Al-Habshy.
3. Maalim Muhammad bin Idriss.
4. Sayyid Muhammad bin Abbas Jamalul-Leyl.
5. Sayyid Abdurrahman bin Sheikh A-Habshy.
6. Ustadh Salum Hemed Saleh.

Baadhi ya faida za uradi huu.

Uradi huu wa Baa-Sawdan una faida nyingi sana, dua nzito zilizomo ndani yake na adhkari tofauti zinaufanya uradi huu kuwa na manufaa makubwa kwa mwenye kuusoma.

Uradi huu zaidi humlinda mtu na maadui wa kila namna, mahasidi, wachawi, madhalimu, wenye chuki n.k

Utukufu na baadhi ya sifa zake

Sayyid Ahmad bin Husein alipendwa na watu wa namna zote na kuheshimiwa sana. Wanavyuoni walioishi zama zake walimtanguliza na khasa katika kuomba dua, walimheshimu sana na wengine walimsifu

kwa sifa za UchaMungu wa hali ya juu kabisa. Nae akiwatukuza Wanavyuoni kuanzia Mashekhe zake hadi wale wa rika yake. Sayyid Ahmad alikuwa akimtukuza mno Habib Omar bin Sumeit nae Habib Omar alikuwa akimheshimu na akiashiria kuwa Bwana huyu alikuwa ni katika watu wa "Sirri" wa *dhahir na batin.*

Bwana huyu alikuwa na Karama za wazi na wanayafahamu hayo waliomdiriki, akiwabashiria watu mambo, basi huwafikia yale aliyoyabashiri. Wakati Habib Omar bin Sumeit alipohama Zanzibar kwenda Shihr (moja ya miji ya Hadhramout) baada ya 1964 kwa lengo la kutokurudi tena Zanzibar basi Sayyid Ahmad bin Husein alihuzunika sana na akasema "Hakuna tena raha ya kuishi Zanzibar" basi haukuvuka muda mrefu isipokuwa akafariki dunia!.

Alikuwa mnyenyekevu, mkarimu, hapendi kujitanguliza, mpole, mwenye bashasha kila wakati, akifanya mzaha na wale walio karibu nae, akimdhukuru Mola wake katika hali zake zote na mengi mengineyo yaliyo mazuri.

Watoto wake

Sayyid Ahmad bin Husein hakubahatika kupata mtoto.

Kufariki kwake

Alifariki siku ya Jumatano tarehe 21 Shaabani 1385. Alisaliwa katika Msikiti wa Ijumaa Malindi na Sala iliongozwa na Sayyid Hamid Mansab na kuzikwa ndani ya Quba alimozikwa Habib Ahmad bin Sumeit mmoja kati ya Mashekhe zake.

Rejea

1. *Sheikh Abdallah Saleh Farsy "Baadhi ya Wanavyuoni wa Mashariki ya Afrika" cha mwaka 1972.*
2. *Sayyid AbdulQadir Juneyd "Al-Uqudul-Jahizah".*
3. *Sayyid AbdulQadir Juneyd "Al-Yamaniyyunal Hadhaarim fii Sharq Afriqiya".*
4. *Kutoka kwa baadhi ya waliomdiriki.*

Maahad Juneyd Islamiy - 2018

Kitengo cha Bahthi na Utafiti

+255 777 878 047 – Zanzibar